**ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

**2020 - 2025**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | **Mhe. Zubeir Ali Maulid** | - | **SPIKA** |
| 2. | **Mhe. Mgeni Hassan Juma** | - | **Naibu Spika/Nafasi za Wanawake** |
| 3. | **Mhe. Hemed Suleiman Abdulla** | - | **MBM/Makamu wa Pili wa Rais//Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Uteuzi wa Rais** |
| 4. | **Mhe. Abdalla Hussein Kombo** | - | **Jimbo la Mkoani** |
| 5. | **Mhe. Abdalla Abass Wadi** | - | **Jimbo la Nungwi** |
| 6. | **Mhe. Ali Abdulghulam Hussein** | - | **Jimbo la Jang'ombe** |
| 7. | **Mhe. Ali Suleiman Ameir** | - | **Jimbo la Pangawe** |
| 8. | **Mhe. Ameir Abdalla Ameir** | - | **Jimbo la Mwanakwerekwe** |
| 9. | **Mhe. Anna Athanas Paul** | - | **Uteuzi wa Rais** |
| 10. | **Mhe. Asha Abdalla Mussa** | - | **Jimbo la Mahonda** |
| 11. | **Mhe. Aza Januar Joseph** | - | **Nafasi za Wanawake** |
| 12. | **Mhe. Bahati Khamis Kombo** | - | **Jimbo la Chambani** |
| 13. | **Mhe. Bakari Hamad Bakari** | - | **Jimbo la Wawi** |
| 14. | **Mhe. Bihindi Hamad Khamis** | - | **Nafas iza Wanawake** |
| 15. | **Mhe. Fatma Ramadhan Mohamed (Mandoba)** | | **Nafasi za Wanawake** |
| 16. | **Mhe. Habibu Ali Muhamed** | - | **Jimbo la Mtambwe** |
| 17. | **Mhe. Haji Omar Kheri** | - | **Jimbo la Tumbatu** |
| 18. | **Mhe. Haji Shaaban Waziri** | - | **Jimbo la Uzini** |
| 19. | **Mhe. Hamza Hassan Juma** | - | **Jimbo la Kwamtipura** |
| 20. | **Mhe. Haroun Ali Suleiman** | - | **Jimbo la Makunduchi** |
| 21. | **Mhe. Harusi Said Suleiman** | - | **Jimbo la Wete** |
| 22. | **Mhe. Hassan Hamad Omar** | - | **Jimbo la Kojani** |
| 23. | **Mhe. Hassan Khamis Hafidh** | - | **Jimbo la Welezo** |
| 24. | **Mhe. Hudhaima Mbarak Tahir** | - | **Nafasi za Wanawake** |
| 25. | **Mhe. Hussein Ibrahim Makungu** | - | **Jimbo la Mtoni** |
| 26. | **Mhe. Jamal Kassim Ali** | - | **Jimbo la Magomeni** |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 27. Mhe. | Juma Makungu Juma | - | Jimbo la Kijini |
| 28. Mhe. | Juma Ali Khatib | - | Uteuzi wa Rais |
| 29. Mhe. | Dkt Khalid Salum Mohamed | - | Jimbo la Donge |
| 30. Mhe. | Issa Haji Ussi Gavu | - | Jimbo la Chwaka |
| 31. Mhe. | Kombo Mwinyi Shehe | - | Jimbo la Wingwi |
| 32. Mhe. | Lela Mohamed Mussa | - | Nafasi za Wanawake |
| 33. Mhe. | Machano Othman Said | - | Jimbo la Mfenesini |
| 34. Mhe. | Maryam Thani Juma | - | Jimbo la Gando |
| 35. Mhe. | Masoud Ali Mohammed | - | Jimbo la Ole |
| 36. Mhe. | Mihayo Juma Suleiman | - | Jimbo la Mwera |
| 37. Mhe. | Miraji Khamis Mussa | - | Jimbo la Chumbuni |
| 38. Mhe. | Mohamed Mgaza Jecha | - | Jimbo la Mtambile |
| 39. Mhe. | Mohamed Ahmada Salum | - | Jimbo la Malindi |
| 40. Mhe. | Mudrik Ramadhan Suleiman | - | Jimbo la Bububu |
| 41. Mhe. | Mtumwa Peya Yussuf | - | Jimbo la Bubwini |
| 42. Mhe. | Mussa Foum Mussa | - | Jimbo la Kiwani |
| 43. Mhe. | Mwanaasha Khamis Juma | - | Jimbo la Dimani |
| 44. Mhe. | Mwanaidi Kassim Mussa | - | Nafasi za Wanawake |
| 45. Mhe. | Mwantatu Mbarak Khamis | - | Nafasi za Wanawake |
| 46. Mhe. | Mwanajuma Kassim Makame | - | Nafasi za Wanawake |
| 47. Mhe. | Dkt. Mwinyi Talib Haji | - | Mwanasheria Mkuu |
| 48. Mhe. | Nadir Abdullatif Yussuf | - | Jimbo la Chaani |
| 49. Mhe. | Nassor Salim Ali | - | Jimbo la Kikwajuni |
| 50. Mhe. | Panya Ali Abdall | - | Nafasi za Wanawake |
| 51. Mhe. | Rahma Kassim Ali | - | Nafasi za Wanawake |
| 52. Mhe. | Riziki Pembe Juma | - | Nafasi za Wanawake |
| 53. Mhe. | Rukia Omar Ramadhan | - | Jimbo la Amani |
| 54. Mhe. | Saada Ramadhan Mwendwa | - | Nafas iza Wanawake |
| 55. Mhe. | Dkt. Saada Mkuya Salum | - | Uteuzi wa Rais |
| 56. Mhe. | Saidi Saleh Salim | - | Jimbo la Tumbe |
| 57. 5Mhe. | Sabiha Fil fil Thani | - | Nafasi za Wanawake |
| 58. Mhe. | Salha Mohamed Mwinjuma | - | Nafasi za Wanawake |
| 59. Mhe. | Salma Mussa Bilal | - | Nafasi za Wanawake |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **60. Mhe.** | **Simai Mohammed Said** | **-** | **Jimbo la Tunguu** |
| **61. Mhe.** | **Soud Nahoda Hassan** | **-** | **Jimbo la Paje** |
| **62. Mhe.** | **Suleiman Masoud Makame** | **-** | **Jimbo la Chonga** |
| **63. Mhe.** | **Suleiman Makame Ali** | **-** | **Jimbo la Ziwani** |
| **64. Mhe.** | **Suleima Haroub Suleiman** | **-** | **Jimbo la Kiembe Samaki** |
| **65. Mhe.** | **Sulubu Kidongo Amour** | **-** | **Jimbo la Mkwajuni** |
| **66. Mhe.** | **Shadya Mohamed Suleiman** | **-** | **Nafasi za Wanawake** |
| **67. Mhe.** | **Shaaban Ali Othman** | **-** | **Jimbo la Mpendae** |
| **68. Mhe.** | **Shamata Shaame Khamis** | **-** | **Jimbo la Micheweni** |
| **69. Mhe.** | **Shaib Hassan Kaduara** | **-** | **Jimbo la Chake Chake** |
| **70. Mhe.** | **Tabia Maulid Mwita** | **-** | **Uteuzi wa Rais** |
| **71. Mhe.** | **Yahya Rashid Abdulla** | **-** | **Jimbo la Kwahani** |
| **72. Mhe.** | **Yussuf Hassan Iddi** | **-** | **Jimbo la Fuoni** |
| **73. Mhe.** | **Zaina Abdalla Salum** | **-** | **Nafasi za Wanawake** |
| **74. Mhe.** | **Zawadi Amur Hassan** | **-** | **Jimbo la Konde** |

**Ndg. Raya Issa Msellem** - **Katibu**

## BARAZA LA KUMI

## MKUTANO WA KWANZA

### Kikao Cha Kwanza – Tarehe 08 Novemba, 2020

*(Kikao kilianza Saa 8:00 mchana)*

### WIMBO WA TAIFA

### DUA

*Katibu (Raya Issa Msellem) alisoma Dua*

### TANGAZO LA RAIS LA KULIITISHA BARAZA JIPYA

**Katibu:** Waheshimiwa naomba niwape taarifa kwamba ofisi ya Baraza la Wawakilishi kupitia Katibu limepokea tangazo la Rais la kuitishwa Baraza. Kwa kanuni ya 20 ya kanuni za Baraza la Wawakilishi toleo la 2020, naomba ninukuu " Kanuni ya 20 inaeleza bila ya kuathiri masharti ya Katiba, Mkutano wa Kwanza wa Baraza jipya utaanza tarehe ile ambayo Baraza jipya limeitishwa na Rais kukutana. Vile vile, kanuni ya 21 fasili ya pili inaelekeza kama ifuatavyo:

Mwanzoni mwa Kikao cha Kwanza cha Mkutano wa Kwanza wa Baraza jipya, Katibu atasoma tangazo la kuliita Baraza jipya kukutana kisha tutasoma dua. Waheshimiwa Wajumbe, kwa heshima kubwa sasa naomba nilisome tangazo la Rais la kuita Baraza jipya kukutana. Hati ya kuitisha mkutano wa Baraza la Wawakilishi chini ya kifungu cha 91(1) ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, mimi Dr. Hussein Ali Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uwezo niliopewa chini ya kifungu cha 89(1) na kifungu 91(1) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, naamuru kwamba mkutano wa Baraza la Wawakilishi ufanyike kwa ajili ya kuendelea na shughuli kuanzia tarehe 8 Novemba, 2020 saa nane kamili mchana.

Imetiwa saini na mhuri wa serikali tarehe 7 Novemba, 2020 na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dr. Hussein Ali Mwinyi. Asanteni waheshimiwa naomba mupokee taarifa hiyo ya tangazo la Mhe. Rais wa Zanzibar.

### Uchaguzi wa Spika

**Katibu:** Waheshimiwa Wajumbe, kwa mujibu wa maelekezo ya kifungu cha 73(4) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, yanaeleza kuwa hakuna shughuli yoyote ya Baraza itakayoendelea wakati kiti cha Spika kipo wazi. Kwa hivyo, ajenda ya kwanza kabisa ni uchaguzi wa Mhe. Spika. Waheshimiwa wajumbe, kwa mujibu wa kanuni ya 5 ya kanuni ya Baraza la Wawakilishi Toleo la mwaka 2020 kwa heshima kubwa naomba niwaeleze kuwa kazi inayowakabili mbele yenu ni kumchagua Spika wa Baraza la Wawakilishi la Kumi ambayo mutaifanya muda mfupi ujao kwa kupiga kura. Kwa mujibu wa Katiba kura za Wajumbe za kumchagua Spika zitakuwa za siri.

Napenda kuwaatarifu kuwa Katibu wa Baraza la Wawakilishi amepokea kutoka Tume ya uchaguzi majina matano ya wagombea ya nafasi ya Spika ambayo la kwanza, Mhe. Ali Makame Issa kutoka chama cha CUF, wa pili Mhe. Ameir Hassan Ameir kutoka Chama cha Demokrasia Makini, wa tatu Mhe. Hamad Mohammed Ibrahim kutoka chama cha UPDP, wa nne ni Mhe. Naima Salum Hamad kutoka chama cha UDP na watano Mhe. Zubeir Ali Maulid kutoka chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Waheshimiwa baada ya kuwatambua wagombea hao, naomba kwa mukhtasari nieleze utaratibu wa uchaguzi wa Mhe. Spika.

Kwa mujibu wa kanuni ya Baraza la Wawakilishi ya mwaka 2020 ili tuweze kutekeleza kazi hiyo kwa ufanisi kabla ya zoezi la kupiga kura kuanza, wagombea watapewa nafasi ya kujieleza mbele yenu kwa muda usiozidi dakika tano na mnaweza kumuuliza mgombea maswali yasiozidi matatu. Baada ya hapo wajumbe mtapatiwa karatasi za kupigia kura ambapo kila mjumbe atapewa karatasi moja ambayo utahakikisha imewekwa muhuri nyuma yake na unachotakiwa kufanya ni kuweka alama ya vyema tu kwenye sehemu husika. Ukimaliza unaikunja vizuri karatasi hiyo na kuitumbukiza kwenye masanduku ambayo yatapitishwa na wahudumu wetu. Itakapotokezea kwamba mjumbe kabla ya shughuli ya kupiga kura kumalizika amekosea kujaza karatasi ya kura ataruhusiwa kuirudisha kwa Katibu karatasi hiyo na Katibu ataiharibu mara moja ili karatasi iliyoharibika na mjumbe huyo atapewa karatasi nyengine kwa ajili ya kuendelea na zoezi la kupiga kura.

Waheshimiwa Wajumbe baada ya Katibu kuridhika kwamba wajumbe wanaotaka kupiga kura wamemaliza kupiga kura atazikusanya kura hizo kuzihesabu na hatimae atatangaza matokeo. Mgombea anaruhusiwa kushuhudia yeye mwenyewe au kuweka wakala wakati wa kuhesabu kura. Ushindi utakuwa ni kwa mjumbe aliepata kura nyingi zaidi ya wagombea wengine, baada ya maelezo hayo mafupi naomba sasa nimkaribishe mgombea wetu wa kwanza Mhe. Ali Makame Issa kutoka chama cha wananchi CUF. Mheshimiwa huyu baada ya kufika tutamuomba atumie muda usiozidi dakika tano kujieleza mbele yenu na baadae kama mtapenda mnaweza kumuuliza maswali yasiozidi matatu ili tuendelee na mgombea mwengine baada ya hapo, wahudumu naomba mumpatie taarifa na mumuingize mgombea wetu Mhe. Ali Makame Issa.

**Mhe. Ali Makame Issa:** Ahsante sana, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma kwa kupata fursa hii adhimu ya kuja katika ukumbi huu kuomba nafasi ya kugombea Uspika wa Baraza la Wawakilishi. Kama ilivyotangulia jina langu ni Ali Makame Issa kutoka Chama cha Wananchi *CUF*. Leo hii nasimama hapa ikiwa ni siku moja ya historia kubwa sana kwangu mimi kwa taifa langu. Ndugu Wajumbe naamini muda mfupi unaofuata mtakuwa Wawakilishi kamili baada ya kula kiapo cha utiifu, sababu ambazo kuwa zimenileta hapa kuja kugombea nafasi hii, ni kutimiza vigezo ambavyo vimetakiwa na Tume ya Uchaguzi kama walivyotaka kwamba mtu yeyote mwenye sifa za kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa sifa zinazojulikana, anaweza akajaza fomu ya kugombea nafasi ya kuwa Spika. Waheshimiwa, pamoja na yote kama mnavyofahamu nchi yetu kila baada ya miaka mitano hufanyika jambo hili kubwa kwa maslahi ya taifa na mimi kwa sababu ni mzanzibari mwenye nia njema na Zanzibar mwenye kuwatakia mazuri Wazanzibari nimeamua kuchukua fursa hii bila kujali itikadi yangu

ya chama, bila ya kujali umri wangu au uwezo wangu lakini kwa sababu naamini ninao uwezo wa kulitumikia au kuitumikia nafasi hii kwa kufuata kanuni na sheria ambazo kuwa zinawekwa katika Baraza na naamini naweza nikafanya hayo kwa uadilifu mkubwa kwa mujibu wa sheria na kanuni za Baraza la Wawakilishi.

Waheshimiwa Wajumbe, pamoja na kugombea nafasi hii naamini nafasi kupatikana mara baada ya uchaguzi na mwisho wa siku Baraza likaanza vikao vyake likiongozwa na Spika wa Baraza la Wawakilishi.

**Katibu:** Mheshimiwa malizia dakika zako tayari zimemaliza.

**Mhe. Ali Makame Issa:** Waheshimiwa Wajumbe, naamini wazanzibari ni jamii kama jamii nyengine pamoja na yote ninachowaomba wajumbe wote munipigie kura bila ya kujali itikadi zenu za vyama, bila kujali kwamba huyu anatoka wapi. Kwa sababu wito ambao kuwa nimetikia hapa ni kutokana na Rais aliechaguliwa kuwahimiza wazanzibari kwamba tuweze kuunganishwa kwa pamoja kwa maslahi ya taifa na mimi naamini hii ndio ngome ya wazanzibari. Hichi ndio kituo cha wazanzibari wanategemea kutatuliwa matatizo yao, wanategemea mema kutoka katika sehemu hii.

**Katibu:** Mheshimiwa malizia.

**Mhe. Ali Makame Issa:** Kwa haya ambayo nimeyazungumza nawaomba waheshimiwa ndugu zangu Wawakilishi ambao kuwa wote waliopo hapa ni kutoka CCM naamini isipokuwa mmoja wa TADEA, naomba kura zenu nyote ili niwe Spika wenu.

**Katibu:** Ahsante Muheshimiwa tuna muda wa maswali kama kuna mjumbe yeyote ambae anataka kumuuliza maswali. Ahsante sana Muheshimiwa tunakushukuru tunaomba uwende ukasubirie nje tupate kuendelea na zoezi.

Naomba nimuite Mhe. Ameir Hassan Ameir kutoka chama cha Demokrasia Makini. Wahudumu naomba mumuingize Mhe. Ameir Hassan Ameir ili na yeye apate nafasi ya kujieleza. Tufanye haraka. Mhe. Ameir Hassan Ameir kutoka Demokrasia Makini karibu sana mbele yako ni wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wapo kukusikiliza wewe kwa nafasi ambayo umegombea ya uspika. Una dakika tano za kujieleza na katika dakika hizo unatakiwa uombe kura kwa wajumbe, karibu mheshimiwa.

**Mhe. Ameir Hassan Ameir:** Ahsante, Katibu Wa Baraza na meza kuu. Waheshimiwa Wajumbe Wawakilishi wateule mabibi na mabwana, Asalaam Aleykum wakubwa shikamooni akiwemo mwalimu wangu maalim Haroun. Kwa jina naitwa Ameir Hassan Ameir ni Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia Makini Tifa. Kwa bahati nzuri nilikuwa ni miongoni mwa wagombea kumi na saba wa urais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Niende haraka haraka kwanza nishukuru, nishukuru kwa kupata nafasi hii kwa mara ya kwanza kusimama hapa mbele yenu Waheshimiwa Wawakilishi wateule kwa mininajihi ya kuomba kura ili niwe Spika kuliendesha Baraza hili la kumi la Wawakilishi la Zanzibar. Kwa kifupi, kama nilivyosema mwanzo jina langu ni Ameir Hassan Ameir nimezaliwa miaka 39 iliopita na elimu yangu nimesoma

Stashahada ya Menenjimenti ya Biashara lakini vile vile nina *pre-degree ya child right protection.* Katika uwongozi mimi nina uzoefu wa kuwa Katibu Mkuu wa chama kwa muda wa miaka 15 mpaka sasa hivi.

Niwaambie waheshimiwa endapo mutanipa kura zenu Waheshimiwa Wajumbe, nitahakikisha Baraza hili la Wawakilishi kwanza kulinda maslahi ya wajumbe. Labda niwaambie kuwa nafahamu changamoto za mishahara lakini nikwambieni kuhusiana na mishahara ambapo mutanipa kiti cha kuwa Spika nitahakikisha kwamba mishahara yenu inakuwa ni mizuri zaidi. Lakini sio hilo tu, vile vile nitahakikisha yale maposho.

**Katibu:** Bado dakika yako moja malizia uombe kura.

Kwa bahati mbaya muda sio rafiki lakini nitahakikisha kudumisha umoja wa mabunge mengine ili wajumbe wapate nafasi ya kwenda kusoma katika Commonwealth na mabunge mengine ili kuhakikisha kwamba Wawakilishe wetu wawe na falsafa nzuri ya kumsaidia Mhe. Rais wa awamu ya nane, nawaombeni wote mnipe kura na hasa Mhe. Juma Ali Khatib na Issa Haji Ussi ahsanteni sana.

**Katibu:** Ahsante sana Mhe. Ameir Hassan Ameir tunakushukuru sasa hivi ni nafasi ya wajumbe kukuuliza na wanaweza kukuuliza masuala matatu. Ahsante wamekuelewa tusubiri nje.

Naomba sasa nimuite Mhe. Hamad Mohammed Ibrahim wa *UPDP* tafadhali wahudumu muongozeni, Mhe. Hamad Mohammed Ibrahim kutoka chama cha *UPDP* karibu sana Baraza la Wawakilishi lakini mbele yako ni wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wanakusikiliza una dakika tano za kujieleza na baada ya hapo sasa unatakiwa katika hizo dakika tano kuomba kura, ukimaliza watapata nafasi ya kukuuliza maswali matatu kama watakuwa nayo ahsante karibu unaweza kujieleza na kuomba kura.

**Mhe. Hamad Mohammed Ibrahim:** Ahsante asalam aleykum ndugu zangu, kwa jina naitwa Hamad Mohammed Ibrahim natokea chama cha *United Peoples Democratic Party* (*UPDP*) nimekuja hapa kwa niaba ya Chama changu, nimepata ridhaa ya Chama hicho cha UPDP kuja kugombea nafasi hii ya Uspika, katika Baraza letu hili tukufu. Nimetolewa na chama changu kwa sababu nina uwezo wa kufanya hivyo ni mzoefu katika mambo mbali mbali ya kisiasa.

Mwaka 2010 Chama changu kiliniteua kuwa Katibu Mkuu wa Chama 2010/2015 mwaka 2015 nimepata tena hiyo nafasi, lakini mwaka 2020 pia nimeteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa chama changu kwa maana hiyo nina uzoefu kwa mambo haya.

Lakini mwaka 2010 hiyo hiyo niligombea katika nafasi ya Umakamo wa Rais Mbunge mwenza kupitia chama changu, nikapata tena ridhaa hiyo mwaka 2015 kama mgombea mwenza, kwa maana hiyo nina uzoefu mkubwa ndio maana leo nimekuja kuonana na ndugu zangu rangi ya kijani hapa wanichague kuwa Spika wa Baraza hili. Lakini nimekuwa Katibu wa vikao vyote vya chama changu vikao vikubwa vile kuanzia kamati tendaji, kamati kuu na Halmashauri kuu pamoja na Mkutano Mkuu nisehemu ya kwamba nina uzoefu wa hali ya juu wa kisiasa kusimamia mambo mbali mbali.

Kwa ajili ya kufupisha muda tu naomba basi ridhaa zenu munichague kuwa Spika wa Baraza hili ili tushirikiane katika kuleta ufanisi hapa nchini kwetu ahsanteni sana.

**Katibu:** Ahsante Mheshimiwa naomba niwape nafasi Waheshimiwa wajumbe kama mna maswali yoyote ya kumuuliza, nakushukuru Mheshimiwa wamekusikia na naomba ukatusubirie ili tuendelee na zoezi linalofuata ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa sasa naomba nimuite Mhe. Naima Salum Hamad kutoka chama cha UDP karibu wahudumu muongozeni.

Mhe. Naima Salum Hamad karibu sana Baraza la Wawakilishi na mbele yako ni wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wako kwa ajili ya kukusikiliza na unaweza kutumia dakika tano kwa ajili ya kujieleza pamoja na kuomba kura, badala ya hapo wanaweza kukuuliza maswali kama watakuwa nayo karibu dakika tano kwa ajili ya kazi hiyo.

**Mhe. Naima Salum Hamad:** Assalamu aleykum ndugu Waheshimiwa kwa jina naitwa Naima Salum Hamad kutoka chama cha *UDP* nikiwa Katibu wa Kinamama taifa, pia ni Katibu wa Mkoa mpaka sasa hivi. Tarehe 28/10/2020 niligombea Ubunge Jimbo la Mfenesini sikufanikiwa, lakini pia leo nasimama hapa kugombea Uspika kama mama, naomba kura zenu naomba mashirikiano yenu ili tushirikiane kuendesha Baraza hili kwanza niwaulize nani kama mama.

**Waheshimiwa:** Hakuna.

**Mhe. Naima Salum Hamad:** *Inshaallah* naomba nione thamani ya mama naomba mashirikiano yenu inshaallah.

**Katibu:**Ahsante Mheshimiwa wemekuelewa na tunaomba urudi utapata utaratibu mwengine.

Waheshimiwa Wajumbe wa mwisho katika zoezi hili ni Mhe. Zubeir Ali Maulid kutoka chama cha CCM naomba wahudumu mumuite pamoja na kumuongoza karibu Mheshimiwa.

*(Hapa watendaji walikwenda kumtafuta Mhe. Zubeir Ali Maulid mgombea wa Uspika)*

*(Hapa watendaji wa Baraza waliingia na Mhe. Zubeir Ali Maulid ndani ya ukumbi*

*wa Baraza la Wawakilishi)*

**Katibu:** Mhe. Zubeir Ali Maulid kutoka Chama cha Mapinduzi *(CCM)* karibu katika Baraza la Wawakilishi tunakupa dakika tano za kujieleza pamoja na kuomba kura mbele yako ni wajumbe wanakusikiliza karibu.

**Mhe. Zubeir Ali Maulid:** Ahsante sana, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi niliyesimama mbele yenu naitwa Zubeir Ali Maulid ndie Spika ambae niliemaliza muda wangu, lakini nimesimama hapa kuomba ridhaa yenu kwa kipindi chengine cha muhula wa pili. Kazi nilizozifanya nikishirikiana nanyi wote mnazifahamu sina haja ya kutoa maelezo mengi sana.

Mimi naomba niuokoe muda kwa kukuombeni kura zenu zote ahsanteni sana Waheshimiwa.

**Katibu:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa kujieleza na kwa kuokoa muda Waheshimiwa Wajumbe mmemsikia Mhe. Zubeir Ali Maulid kama mna maswali. *(Makofi)*

**Wajumbe**: Hakuna.

**Katibu:** Ahsante sana Mheshimiwa wamekusikia na tunakushukuru tunaomba utupishe tuendelee na shughuli nyengine.

*(Mhe. Zubeir Ali Maulid alitoka nje ya ukumbi kwenda kusubiri zoezi la uchaguzi)*

**Katibu:** Waheshimiwa Wajumbe baada ya zoezi hilo tunaomba tuendelee na zoezi la kupiga kura na wahudumu wetu watatoa karatasi za kura tutaendelea na utaratibu ahsante.

Waheshimiwa Wajumbe idadi ya Wajumbe wetu waliohudhuria hapa na watakaopiga kura ni 70 ahsanteni na naomba tuendelee na zoezi.

**Uchaguzi wa Spika**

*(Hapa Waheshimiwa Wajumbe waligaiwa karatasi za kura)*

Waheshimiwa Wajumbe tunaanza zoezi la kukusanya kura boksi moja litapita huku na jengine litapita huku, waonyeshe kwanza kama lipo tupu sawa. Kuna waliokosa kura jamani wajumbe.

**Katibu:** Waheshimiwa Wajumbe naomba niwataarifu kwamba zoezi la upigaji kura limemaliza na tutaakhirisha Baraza kwa ajili ya kwenda kuhesabu, Waheshimiwa Wanne waliotangulia ukiachia Mhe. Zubeir Ali Maulid wamekiamini kiti katika uhisabuji wa kura**,** lakini Mhe. Zubeir Ali Maulid amempa uwakala Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis, kwa hivyo utafuatana nae na naomba tuakhirishe kidogo kwa ajili ya zoezi hili ahsanteni.

*(Saa 8.20 mchana Baraza liliahirishwa kwa muda kuhesabu kura)*

*(Saa 8.25 mchana Baraza lilirudia)*

**Matokeo ya Uchaguzi wa Spika**

**Katibu:** Waheshimiwa Wajumbe baada ya zoezi letu la uchaguzi wa Mhe. Spika, tunaomba kuwatangazia matokeo ya uchaguzi wa Spika wa Baraza la Wawakilishi, uliofanyika leo tarehe 8/11/2020.

Maelezo ya matokeo hayo wajumbe waliopiga kura kati ya wajumbe wote waliohudhuria ni (70)

| | | | |
|---|---|---|---|
| Kura zilizoharibika | - | 0 | |
| Kura halali | - | 70 | |
| Kura zilizomkubali Mhe. Ali Makame Issa Kutoka chama cha *CUF* | | - | 0 |
| Kura zilizomkubali Mhe. Ameir Hassan Ameir Demokrasia Makini | | - | 0 |
| Kura zilizomkubali Mhe. Hamad Mohammed Ibrahim kutoka *UPDP* | | - | 0 |
| Kura zilizomkubali Mhe. Naima Salim Hamad kutoka *UDP* | | - | 0 |
| Kura zilizomkubali Mhe. Zubeir Ali Maulid kutoka CCM | | - | 70 |

Kwa hivyo Mhe. Zubeir Ali Maulid wa CCM amechaguliwa kuwa Spika wa Baraza la Wawakilishi kwa asilimia mia moja (100%) kwa kipindi cha mwaka 2020/2025 ahsanteni.

**Wajumbe:** CCM, CCM, CCM.

**Katibu:** Waheshimiwa Wajumbe naomba tuendelee na zoezi, wahudumu naomba kumuita Mhe. Zubeir Ali Maulid kuja mbele hapa ya Baraza na kula kiapo cha Spika. Wahudumu naomba mumuongoze Mhe. Spika.

*(Hapa wahudumu walikwenda kumtafuta Mhe. Spika na Mhe. Mohamed Ahmada Salum kuingia naye katika Baraza kwa ajili ya kula kiapo)*

**Katibu:** Mhe. Zubeir Ali Maulid ninayo heshima kukutaarifu kwamba Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi katika kutekeleza Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 na katika kutumia haki na fursa walizopewa kwa mujibu wa Sheria wamekuchagua wewe uwe Spika wa Baraza hili, kutokana na kuchaguliwa kwako huko sasa nakuita wewe Mhe. Zubeir Ali Maulid uape kiapo cha uaminifu ukisha ukalie kiti cha Baraza hili ukiwa Spika, karibu sana Mheshimiwa.

## KIAPO CHA MHE. SPIKA

**Mhe. Spika:** Mimi Zubeir Ali Maulid naapa kwamba nitakuwa muaminifu kwa Zanzibar katika kazi zangu za Uspika na nitaitumikia kwa moyo wangu wote na kwamba nitazihifadhi, nitazilinda na kuzitetea kwa dhati Katiba ya Zanzibar na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Nakuomba Mwenyezi Mungu unisaidie.

**Katibu:** Mhe. Spika, naomba kukukabidhi mkoba huu ambao ndani yake mna vitendea kazi vya kazi yako ya Baraza la Wawakilishi kama ukiwa Spika, ndani yake kuna Katiba ya Zanzibar, Katiba ya Jamhuri ya Muungano, kuna Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo la 2020, pia kuna sheria mbali mbali ambazo zinawahusu Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi pamoja stahiki za wajumbe ukiwemo wewe Mhe. Spika, naomba upokee.

Wahudumu naomba mumuongoze Mhe. Spika, kwa ajili ya kukalia kiti chake. Karibu Mhe. Spika.

*(Hapa Mhe. Spika aliapa na kukalia kiti chake)*

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi nichukue nafasi hii kwanza nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwepo hapa leo tukiwa wazima wa afya na kuweza kukamilisha jambo letu hili la kikatiba.

Lakini pia nichukue nafasi hii waheshimiwa nikushukuruni sana na nyinyi waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi pia nikupongezeni sana mliotokea kwenye majimbo na wale ambao wamekuja kwa kupitia viti maalum pamoja na wale wateule, nakupeni sana pongezi na nashukuru kwa kazi kubwa sana ambayo mmeifanya.

Nichukuwe nafasi hii kwa ufupi pia kwanza niwashukuru wazee wangu. Baba yangu mzazi Marehemu Ali Maulid Simai Mwenyezi Mungu amlaze mahala pema lakini pia mama yangu Bi Hanifa Adam na yeye Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema. Lakini pia nichukuwe nafasi hii kuishukuru sana familia yangu, wake zangu Fatma Abdalla Mzee na Warda Haji Mwadini na bila shaka kama wapo wanaweza wakasimama huko juu mkawaona. *(Makofi)*

Lakini pia naomba nitambue na kuwashukuru vile vile wanangu na naomba niwataje Abdulkarim Zubeir, Hanifa Zubeir, Zahran Zubeir, Zahor Zubeir na Zaurat Zubeir. Siwaoni kwenye *gallery* lakini Insha'Allah mtakuja kuwaona siku ambayo watakuwepo, najua wapo.

Waheshimiwa Wajumbe baada ya shukurani hizi naomba pia nikishukuru changu Chama cha Mapinduzi nakishukuru kwa kuniamini lakini nichukuwe nafasi hii kukipongeza kwa ushindi ambao wameupata safari hii, ni ushindi mkubwa ambao sasa wananchi wametukopesha wametupa ushindi mkubwa lakini matarajio yao kwetu ni makubwa vile vile, kwa hiyo *Inshaallah* Mwenyezi Mungu ajaalie tufanye kazi kubwa ya kuwaridhisha kwamba kile tulichokiahidi tutaweza kukifikisha na *Inshaallah* kwa kushirikiana tutaweza kulifanikisha hilo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe baada ya shukrani hizo naomba sasa nichukuwe nafasi ya kumwita katibu ili tujuwe shughuli inayofuata ili tuweze kuendelea na shughuli zetu.

## KIAPO CHA UAMINIFU

Wajumbe wafuatao waliapishwa kiapo cha uaminifu na baada ya kumaliza walikaa katika nafasi zao.

Mhe. Anna Athanas Paul
Mhe. Hemed Suleiman Abdalla
Mhe. Juma Ali Khatib
Mhe. Saada Mkuya Salum
Mhe. Tabia Maulid Mwita
Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed
Mhe. Abdalla Hussein Kombo
Mhe. Abdalla Abasi Wadi
Mhe. Ali Abdulghullam Hussein

Mhe. Ali Suleiman Ameir
Mhe. Ameir Abdalla Ameir
Mhe. Asha Abdalla Mussa
Mhe. Aza Januar Joseph
Mhe. Bahati Khamis Kombo
Mhe. Bakari Hamad Bakari
Mhe. Bihindi Hamad Khamis
Mhe. Fatma Ramadhan Mohamed (Mandoba)
Mhe. Haji Omar Kheri
Mhe. Haji Shaaban Waziri
Mhe. Hamza Hassan Juma
Mhe. Haroun Ali Suleiman
Mhe. Harusi Said Suleiman
Mhe. Hassan Khamis Hafidh
Mhe. Hudhaima Mbarak Tahir
Mhe. Hussein Ibrahim Makungu
Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)
Mhe. Jamal Kassim Ali
Mhe. Juma Makungu Juma
Mhe. Jamal Kassim Ali
Mhe. Juma Makungu Juma
Mhe. Leila Mohamed Mussa
Mhe. Machano Othman Said
Mhe. Maryam Thani Juma
Mhe. Masoud Ali Mohammed
Mhe. Mgeni Hassan Juma
Mhe. Mihayo Juma Suleiman
Mhe. Miraji Khamis Mussa
Mhe. Mohamed Mgaza Jecha
Mhe. Mohamed Ahmada Salum
Mhe. Mudrik Ramadhan Suleiman
Mhe. Mtumwa Peya Yussuf
Mhe. Mussa Foum Mussa
Mhe. Mwanaasha Khamis Juma
Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa
Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis
Mhe. Mwanajuma Kassim Makame
Mhe. Dkt. Mwinyi Talib Haji
Mhe. Nadir Abdullatif Yussuf Alwardy
Mhe. Nassor Salim Ali
Mhe. Panya Ali Abdalla
Mhe. Rahma Kassim Ali
Mhe. Riziki Pembe Juma
Mhe. Rukia Omar Ramadhan
Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa

Mhe. Saada Mkuya Salum
Mhe. Saidi Saleh Salim
Mhe. Sabiha Filfil Thani
Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma
Mhe. Salma Mussa Bilal
Mhe. Simai Mohammed Said
Mhe. Soud Nahoda Hassan
Mhe. Suleiman Masoud Makame
Mhe. Suleiman Makame Ali
Mhe. Suleiman Haroub Suleiman
Mhe. Sulubu Kidongo Amour
Mhe. Shadya Mohamed Suleiman
Mhe. Shaaban Ali Othman
Mhe. Shamata Shaame Khamis
Mhe. Shaib Hassan Kaduara
Mhe. Yahya Rashid Abdulla
Mhe. Yussuf Hassan Iddi
Mhe. Zaina Abdalla Salum
Mhe. Zawadi Amur Nassor

**Katibu Mezani (Ndugu Mussa Kombo Bakari):** Mhe Spika, naomba kutoa taarifa kwamba tumemaliza zoezi la kuwaapisha Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, ukiondoa majina manne ambayo wajumbe baada ya kuitwa hawakuonekana katika Ukumbi wa Baraza la Wawakilishi. Kwa waliokuwepo tumemaliza zoezi la kuwaapisha wajumbe wote, nashukuru Mheshimiwa.

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, kwanza nichukue nafasi hii kukupongezeni sana nyote. Nikupongezeni kwa kuwa nyote sasa mmeshakuwa ni Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kamili kwa vile nyote mmeshakula kiapo cha uaminifu. (*Makofi)*.

Kwanza kabisa, nichukue nafasi hii nitambue ushiriki wa waheshimiwa wafuatao ambao nimegombea nao kwenye nafasi ya Uspika naomba nitambue uwepo wao hapa nianze na:

1. Mhe. Ali Makame Issa — kutoka Chama cha *CUF*
2. Mhe. Naima Salum Hamad — kutoka Chama cha *UDP*
3. Mhe. Ameir Hassan Ameir — kutoka Chama cha Demokrasia Makini
4. Mhe. Hamad Mohammed Ibrahim — kutoka Chama cha *UPDP*

Waheshimiwa wametekeleza wajibu wao wa kikatiba wameshiriki kwenye mchakato huu wa kupatikana kwa Spika, tunashukuru sana kwa ushiriki wao, lakini pia huo sio mwisho wajue kwamba Chama cha Mapinduzi kitaendelea kushirikiana na kila mtu ambaye yupo tayari kushirikiana nacho. Kwa hiyo, wao wote ni sehemu ya kujenga nchi yetu. (*Makofi)*.

Baada ya shukurani hiyo naomba nitoe matangazo mafupi, kwanza kabisa naomba niwatangazie Waheshimiwa Wajumbe wote ambao hawajajisajili wafike katika sehemu za usajili hapo nje, ili waweze kukamilisha hilo zoezi.

Pia, Wajumbe ambao hawakukamilisha taarifa zao katika fomu za usajili, wanaombwa sana wakamilishe taarifa hizo. Aidha, wajumbe wote kutoka majimboni wanatakiwa kuleta nakala za vyeti vyao vya ushindi walivyokabidhiwa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar. Tunawaomba sana waheshimiwa tuweze kulifanikisha zoezi hili. Ahsanteni sana.

Tangazo linalofuata ni tangazo la wageni, wageni wa Mhe. Spika wa Baraza la Wawakilishi, naomba nitambue Mhe. Dkt. Abdalla Hasnuu Makame, naona hajafika. Naomba nimtambue Bi Susiat Hussein Hamza, naomba nitambue uwepo wa Ndg. Wardat Haji Mwadini.

Vile vile, naomba utambuzi wa wanangu:

1. Abdulkarim Zubeir
2. Hanifa Zubeir
3. Zahor Zubeir
4. Zahran Zubeir
5. Zaurat Zubeir

Naomba pia nitambue uwepo wa wageni wote waliokuja kushuhudia wawakilishi wao wakiapishwa, nitambue uwepo wenu karibuni sana Baraza la Wawakilishi.

Baada ya tangazo hilo sasa naomba nimwite katibu kama kuna jambo lolote. Samahani Waheshimiwa Wajumbe, kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 74 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 nikisoma pamoja na kanuni ya saba na ya nane ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo la mwaka 2020. Yanatutaka kuchagua Naibu Spika katika Mkutano wa Kwanza baada ya kuvunjwa kwa Baraza au katika Mkutano wa Kwanza wa Baraza endapo kiti cha Naibu Spika kitakuwa wazi.

Hivyo, Waheshimiwa Wajumbe, naomba kuwataarifu rasmi kuwa uchaguzi wa Naibu Spika utafanyika siku ya Jumanne tarehe 10/11/2020 saa nane kamili za mchana. Waheshimiwa Wajumbe, kila chama cha siasa chenye wajumbe katika Baraza kinaweza kupendekeza jina la mgombea kiti cha Naibu Spika na fomu za uteuzi zinapatikana katika Afisi ya Katibu wa Baraza.

Ikumbukwe kuwa fomu hizo zitajazwa na mgombea wa nafasi hiyo na kuzirejesha kwa Katibu wa Baraza angalau masaa 24 kabla ya uchaguzi huo. Kwa muktadha huo, saa nane kamili mchana ndio mwisho wa kuwasilisha fomu hizo kwa katibu ahsanteni sana.

Waheshimiwa nina taarifa hapa kwamba Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi amemchagua Mhe. Hemed Suleiman Abdalla. (*Makofi).*

Waheshimiwa Wajumbe, sikuwahi kuikamilisha kuitoa lakini hiyo shangwe ni kwamba Mhe. Hemed Suleiman Abdalla amekuwa Makamu wetu wa Pili wa Rais, nami sasa nichukue nafasi hii kwanza kumpongeza sana Mhe. Hemed Suleiman Abdalla, kwa nafasi hiyo ambayo ameipata baada ya kuteuliwa na Mhe. Rais wa Zanzibar na kwa shangwe hiyo Mheshimiwa maana yake

Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi watakuwa na mashirikiano ya karibu sana na wewe katika kuwatumikia wananchi. Karibu sana Mheshimiwa tunakupongeza sana.

**Katibu:** Mhe. Spika, naomba kutoa taarifa kwa Baraza lako tukufu kwamba, shughuli zote tulizozipanga leo zimekamilika.

**Mhe. Spika:** Ahsante waheshimiwa, baada ya shughuli zote hizo kukamilika, naomba kuakhirisha Kikao cha Baraza la Wawakilishi mpaka tarehe 10 Novemba, 2020 saa 8:00 za mchana. Ahsanteni sana waheshimiwa.

*(saa 10:26 Baraza liliakhirishwa mpaka tarehe 10/11/2020 saa 8:00 mchana)*